JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARAYA MAJI**

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

Meneja RUWASA, Wilaya ya Lushoto, S. L. P 336, Lushoto - Tanga,
**Simu:** +255 (0) 27 266 0114, **Tovuti:** www.ruwasa.go.tz,
**Baruapepe:** lushotodm@ruwasa.go.tz

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KATIKA SKIMU ZA MAJI WILAYA YA LUSHOTO.

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Lushoto kwa niaba ya Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs), inawatangazia nafasi za kazi zifuatazao:-

### 1. FUNDI MKUU WA CHOMBO – NAFASI 15

**a. SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe Raia wa Tanzania na mwenye akili timamu
ii. **ELIMU:** Awe na Cheti cha Elimu ya kidato cha nne au zaidi
iii. **UJUZI:** Awe na Cheti cha Fundi Sanifu Maji (Technician) Daraja la I, II, III au Fundi Bomba mwenye Stashahada / Astashahada
iv. **UMRI**: Awe na Umri kuanzia miaka 18 – 45
v. **UAMINIFU:** Awe mwaminifu na mwadilifu na asiwe amewahi kushitakiwa na kosa lolote la jinai au kufungwa jela
vi. Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atakayo pangiwa
vii. Awe na uwezo wa kufanya kazi pasipo kusimamiwa na kuwasimamia mafundi wasaidizi pamoja na waajiriwa wengine
viii. Mara baada ya kuajiriwa Awe tayari kuapa kiapo cha uadilifu katika uongozi.

**b. MAJUKUMU YA FUNDI MKUU WA CHOMBO**

i. Atafanya kazi kama Katibu chini ya Kamati ya Maji ya Chombo (Community Water Committee)
ii. Atakuwa ndiye Mtendaji / Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za kiufundi katika Skimu ya Maji ikiwa ni pamoja na kuandaa na kuwasilisha mahitaji ya vifaa na viungo kwa ajili ya matengenezo / ukarabati mdogo mdogo kwa Msimamizi wa Mradi
iii. Ataratibu na kusimamia shughuli zote za matengenezo ya Mradi pale inapotokea hitilafu
iv. Atakuwa ndiye Msimamizi wa Mafundi wasaidizi (local FUNDI) katika maeneo yao ya utekelezaji
v. Kusimamia na kuzingatia ratiba ya utoaji wa huduma ya Maji (mgao) kwa Wateja / Wananchi kama itakavyo kuwa imepangwa
vi. Kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri wa Kitaalamu katika shughuli yote inayohusisha uunganishaji wa Huduma ya Maji kwa Wateja wapya kuanzia hatua

ya ujazaji fomu, makadilio ya gharama / vifaa na upeleekaji wa huduma kwa Mteja / Mwananchi

vii. Kusimamia usafi wa Vituo vya Maji na miundombinu mingine ya Maji katika eneo lake la utekelezaji

viii. Kushiriki katika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Skimu pamoja na mapato na matumizi

ix. Kushiriki katika uhamasishaji wa ushangiaji wa huduma ya Maji, kushiriki katika kutatua na kusuluhisha Migogoro baina ya Mteja / Mwananchi na Chombo

x. Kutekeleza Majukumu mengine kama jinsi atakavyo pangowa na Msimamizi wa Skimu na ngazi nyingine za juu za utawala.

## 2. MHASIBU WA CHOMBO – NAFASI 15

### a. SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe Raia wa Tanzania na mwenye akili timamu.

ii. **ELIMU:** Awe na Cheti cha Elimu ya kidato cha nne au zaidi

iii. **UJUZI:** Awe na Cheti cha Mafunzo ya awali ya Uhasibu (NTA 3) au zaidi

iv. **UMRI:** Awe na Umri kuanzia miaka 18 – 45

v. **UAMINIFU:** Awe mwaminifu na mwadilifu na asiwe amewahi kushitakiwa na kosa lolote la jinai au kufungwa jela

vi. Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atakayo pangiwa

vii. Awe na uwezo wa kufanya kazi pasipo kusimamiwa na kuwasimamia mafundi wasaidizi pamoja na waajiriwa wengine

viii. Mara baada ya kuajiriwa Awe tayari kuapa kiapo cha uadilifu katika uongozi.

### b. MAJUKUMU YA MHASIBU WA CHOMBO

i. Atafanya kazi kama Mhasibu chini ya Kamati ya Maji ya Chombo (Community Water Committee)

ii. Atakuwa ndiye Mtendaji / Msimamizi mkuu wa masuala ya kifedha katika chombo

iii. Kusimamia na kupokea malipo ya Maji (Ankara) na michango mbalimbali ya Wanachama / Wananchi

iv. Kuandaa taarifa za kifedha (mapato na matumizi) za wiki, mwezi, robo, nusu na mwaka mzima na kuziwasilisha kwa Kamati ya Maji ya Chombo

v. Kutunza Vitabu vya fedha, hati za malipo na nyaraka zote za uthibitisho wa mapato, malipo / matumizi ya fedha ikiwa ni pamoja na kutunza kumbukumbu / nyaraka zote za kimanunuzi za Skimu

vi. Kufanya Malipo baada ya kuidhinishwa na Msimamizi Mkuu wa Chombo

vii. Kushirikiana na Msimamizi wa Chombo kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Skimu

viii. Kushiriki katika uhamasishaji wa ushangiaji wa huduma ya Maji, kushiriki katika kutatua na kusuluhisha Migogoro baina ya Mteja / Mwananchi na Chombo

ix. Kutekeleza Majukumu mengine kama jinsi atakavyo pangiwa na Msimamizi wa Skimu na ngazi nyingine za juu za utawala

**MASHARTI YA KAZI / MSHAHARA**

i. Kazi hii ni ya Mkataba, Mkataba unaweza kuhuishwa na Mwajiri (Chombo) kutokana na utendaji kazi mzuri wa mhusika
ii. Malipo ya Mshahara kwa Mwajiriwa yatatokana na makusanyo / mauzo ya Maji ya Chombo husika
iii. Mwombaji awe tayari kufanya kazi katika vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) katika Eneo atakalopangiwa.

**MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIWA**

i. Maombi yote yaandikwe kwa mkono na yaambatanishwe na Wasifu wa Mwombaji (CV – Maelezo binafsi) yenye Majina 3, Anuani na namba za simu
ii. Nakala za Vyeti vya Ujuzi na kidato cha nne
iii. Picha ndogo 2 (passport size za rangi) za hivi karibuni
iv. Kivuli cha utambulisho wa Uraia ama Kadi ya Mpiga kura
v. Majina ya Wadhamini (Referees) wawili (2) na mawasiliano yao (Anuani na simu).

**NB:** Barua zote za maombi zilizofungwa vizuri kwenye bahasha ziitumwe kwa anuani ifuatayo:-

**MENEJA RUWASA,**
**S.L.P. 336,**
**LUSHOTO,**
**TANGA.**

**Au** kuletwa kwa mkono **OFISI ZA RUWASA WILAYA YA LUSHOTO.**

**MWISHO WA KUPOKEA BARUA ZA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni siku ya **Jumatatu** tarehe **14/08/2023** saa **9:30** Alaasiri. Maombi yatakayo wasilishwa baada ya muda huo hayata pokelewa.

Tangazo hili limetolewa na:-

MENEJA WA RUWASA
LUSHOTO

**......................................**
**MENEJA WA RUWASA (W)**
**LUSHOTO**
**KWA NIABA YA VYOMBO VYA UTOAJI HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII (CBWSO)**